### 3.8 Vikwazo Vya Utafiti na Utatuzi Wake

Yapo matatizo kadhaa ambayo yamejitokeza katika utafiti huu. Kwanza ni gharama za utafiti. Mtafiti amekuwa akijitegemea mwenyewe tangu mwanzo wa utafiti huu hadi kufikia hatua hii. Jambo hili limempa mtafiti wakati mgumu wakati akiendelea

na utafiti huu. Hata hivyo, kutokana na umuhimu wa utafiti huu kwa mtafiti na jamii kwa jumla, mtafiti amelitafutia ufumbuzi tatizo hilo kwa kukopa fedha na pia kupunguza baadhi ya matumizi muhimu ili kupata fedha za kuukamilisha utafiti.

Mtazamo hasi wa jamii kuhusu utafiti, nalo ni tatizo jingine lililojitokeza. Kwa mfano, baadhi ya watu walidhani kuwa, utafiti huu ni kama biashara kwa mtafiti, kuwa, mtafiti anajipatia fedha nyingi kutokana na utafiti huu. Kwa hali hiyo, baadhi ya watafitiwa walihitaji kulipwa ndipo watoe ushirikiano uliyohitajika. Ili kulitatua tatizo hilo, mtafiti alijitahidi kuielimisha jamii juu ya umuhimu wa utafiti katika jamii.

# SURA YA NNE

# UWASILISHAJI NA UCHAMBUZI WA DATA

## 4.1 Utangulizi

Matokeo ya utafiti yamegawanyika katika sehemu kuu mbili zinazoakisi madhumuni na maswali yaliyoongoza utafiti huu. Sehemu ya kwanza inahusu methali za Kipare na dhima zake katika kuendeleza elimu ya jadi ya Wapare. Sehemu ya pili, inahusu vipengele vya fani vilivyomo ndani ya methali za Kipare, ambavyo, ndivyo vinavyoziwezesha methali hizo, kukamilisha dhima zake, kwa ufanisi zaidi, ndani ya jamii.

## 4.2 Uwasilishaji wa Data

Uwasilishaji wa data katika kazi hii ya utafiti, umezingatia matokeo ya taarifa za data zilizopatikana, kabla ya uchambuzi. Majibu ya maswali ya udadisi yamewasilishwa kwa kila moja kujitegemea, kwa njiya ya majedwali au maelezo.

Vyote hivyo vimefanyika, ili kuifanya kazi hii ya utafiti ikidhi haja zake.

## 4.3 Uchambuzi wa Data

Data zilizokusanywa kutoka masikani , zimewekwa katika makundi matatu. Ni data zilizotokana na mahojaji, usaili wa ana kwa ana, na machapishi. Data zenye majibu zaidi ya moja, zimeandaliwa na kuainishwa kwenye majedwali zikionesha idadi ya washiriki kulingana na majibu yaliyotolewa. Kila majibu yalijadiliwa peke yake kulenga mada na tatizo la utafiti.

**Jedwali Na. 4.1: Umri wa Watumiaji Wakuu wa Methali za Kipare kwa Sasa**

| Idadi ya washiriki | Waliosema watu wote | % | Waliosem a watoto | % | Waliosema Vijana | % | Walioacha kujibu swali | % | Waliosem a wazee | % |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 253 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 16 | 6 | 237 | 94 |

Kutokana na kielezeo cha jedwali namba 01, majibu ya wahojiwa yameonesha wazi kuwa, kwa sasa watumiaji wakuu wa methali za Kipare katika jamii ya Wapare ni wazee. Hali hii inadhihirisha kuwa, kwa sasa watoto wengi hawapati fursa kubwa ya kuzitumia methali za Kipare kwenye maisha yao ya kila siku, ikilinganishwa na matumizi ya methali hizo kwa wazee.

Vile vile, kutokana na kielezeo cha jedwali namba 01, inaonekana wazi kuwa, urithishaji wa methali hizo kutoka kizazi kimoja hadi kingine unaenda ukipungua. Sababu za kupungua kwa urithishaji wa methali hizo, zimeelezwa kwenye kijisehemu maalumu, baada ya majibu ya swali la pili. Pia, hali hiyo inaashiria kupungua kwa matumizi ya methali za Kipare, na hivyo, kusababisha pengo kubwa katika Fasihi ya Kipare ambayo, ni muhimu sana katika kuendeleza maarifa mema ya Wapare.

Ni ukweli usiofichika kuwa, matumizi ya methali za Kipare kwenye jamii ya Wapre yanaenda yakipungua siku hadi siku. Hivyo, ni wajibu wa jamii nzima ya Wapare, kutilia mkazo matumizi ya fasihi yao, zikiwamo methali, ambazo, ni kitanzu cha fasihi simulizi. Kwa kufanya hivyo, maadili mema yataendelea kurithishwa kwa vizazi vipya, na wakati huohuo, utamaduni mwema utaendelea kuimarishwa na hivyo, kuilinda heshima ya jamii dhidi ya ugeni hasi unaoingia kwa nguvu.

**Jedwali Na. 4.2: Kuongezeka au Kupungua kwa Matumizi ya Methali za Kipare**

| Idadi ya washiriki | Waliosema matumizi yanaongezeka | % | Waliosema matumizi yanapungua | % |
|---|---|---|---|---|
| 253 | 0 | 0 | 253 | 100 |

Kajato, anaeleza kuwa, wazee wa leo, walizitumia methali za Kipare kwa kiwango kikubwa enzi za ujana wao. Kwa sasa hali ni tafauti, vijana na watoto, hawana tena fursa kubwa ya kuzitumia methali za Kipare kama ilivyokuwa kwa wazee wao. Mwingiliano wa lugha na mfumo wa kisomo cha shule, ni miongoni mwa mambo mengi yanayoathiri matumizi ya methali za Kipare, katika maisha yao kila siku.

Kama walimu wa masomo ya lugha wangekuwa Wapare, wanapofundisha methali, wangeweza kuanza na methali za Kipare ndipo wafundishe methali za Kiswahili. Kama ni wageni, hali iliyopo nchini, ni kuvunja mema ya mila na dasturi za jamii. Kutokana na kielezeo cha jedwali namba 02, ni dhahiri kuwa, matumizi ya methali za Kipare kwenye jamii ya Wapare yanazidi kupungua. Watafitiwa wote 253, ambao ni 100%, wamekiri kwamba, matumizi ya methali hizo yanapungua kwenye maisha ya kila siku ya Wapare.

Turufaina, anafafanua kuwa, kupungua kwa matumizi ya methali za Kipare, kwenye jamii ya Wapare, kunaonesha dalili za wazi kwamba, juhudi kubwa zisipochukuliwa, basi, huwenda matumizi ya methali za Kipare. Vile vile, tatizo la kupungua kwa matumizi ya methali za Kipare likifumbiwa macho, maarifa mema ya jadi, yanayopatikana kwenye methali, hayatafahamika wala kutumika. Jambo hilo, litaifanya jamii, izidi kupwaya kimaadili, na hivyo, kujikuta ikipoteza muelekeo

wake thabiti uliyojengwa na wazee wake kwa karne nyingi zilizopita. Mizizi ikishang'oka, jamii itaelea hewani, huku haiko na huko haiko.

**Sababu za kupungua kwa matumizi ya methali za Kipare kwenye jamii ya Wapare**

Watafitiwa wametoa sababu za kupungua kwa matumizi ya methali za Kipare kwenye jamii ya Wapare;

Wazazi hutumia lugha ya Kiswahili kwenye mawasiliano badala ya lugha ya Kipare. Wazazi wengi wamejijengea dhanna kwamba, watoto wanawasiliana vizuri zaidi kwa kutumia lugha ya Kiswahili. Kutokana na hali hiyo, matumizi ya lugha ya Kipare yamepungua kiasi cha kuwafanya watoto wengi wa Kipare, wasiijue vyema lugha yao ya asili ya Kipare. Kajato anaeleza kuwa, athari za ugeni, kwa kisingiziyo cha maendeleo ya sayansi (ulimbe) na teknolojia (utunduizi), kwa mfano, vyombo vya habari vinavyoongezeka kila kukicha, vimekuwa sababu ya kupungua kwa matumizi ya methali za Kipare kwenye jamii ya Wapare kutokana na matumizi mabaya ya vyombo hivyo. Kabla ya kuletwa runinga, na mitandao mingi ya kijamii, muda wa mapumziko baada ya kazi, wazee wa Kipare walikaa na vijana na watoto wao na kuwafundisha.

Msemo, anasema kuwa, vijana wengi kwa sasa, wanathamini zaidi ugeni, na kuzipuuza tamaduni za kwao za asili. Upuuzaji wa asili na utukuzaji wa ugeni, ni pigo kubwa, kwani fasihi za asili, ya Kipare na methali zake zikiwamo, zimekuwa zikipungua umaarufu wake, na hivyo, kuisababishia jamii hiyo myumbo na khasara kubwa sana.

Kutokana na sababu hizo, inaonekana wazi kwamba, Jamii ya Wapare haina budi kutazama upya njia bora za kuendeleza fasihi yao, kwa kuwa, fasihi ni nyenzo kuu ya kurithishia maarifa ya jadi kutoka kizazi kimoja hadi kingine. Fasihi ikiimarishwa vizuri, inasaidia kwa kiwango kikubwa, kuimarisha maadili mema ya jamii ya Wapare na hivyo, kuyafanya maisha yawe sahali zaidi.

Sengo (2016) anaeleza kuwa, Taifa la Tanzania linategemea jamii ndogo ndogo, kwa utambulisho na maadili, kama msitu na mti mmoja mmoja. Makabila yaking'olewa kisiasa au kifisidi, Taifa litabakiya ombwe tupu la kujazwa matope ya kila aina. Makabila si ukabila, kama Wahaya na Wanyakyusa wameng'olewa kifisidi, leo kuna ukabila upya wa vyama vya siasa, mawilaya mapya na majina makubwa ya wakubwa. Na hayo mapya, hayana maadili mema.

**Jedwali Na. 4.3: Mafunzo Yanayotolewa Kupitia Methali**

| Idadi ya washiriki | Ambao hawakuelezea mafunzo yanayotolewa kupitia methali | % | Walioelezea mafunzo yanayotolewa kupitia methali | % |
|---|---|---|---|---|
| 253 | 17 | 07 | 236 | 93 |

Watafitiwa miambili thelathini na sita (236), ambao ni sawa na asilimia tisini na tatu (93 %), wameweza kutaja na kuelezea mafunzo muhimu yanayotolewa kupitia methali. Mafunzo hayo ni:

Maadili mema, mwenendo mwema, ambao, unakubalika kwenye jamii. Miongoni mwa mafunzo muhimu yanayopatikana kwenye methali za Kipare ni mwenendo mwema, tabia njema zinazokubalika kwenye jamii, kulingana na mila na dasturi zilizomo. (Mbazi).

Mfano;

*Methali; Kuomana na mkwe, ni kuthova ng'ombe.*

*Tarijama; Kugombana na mkwe, ni kukosa ng'ombe.*

Dhima kuu ya methali hiyo, ni kuhimiza kuishi kwa amani na upendo kwenye jamii. Amani na uelewano mzuri kwenye jamii ni muhimu sana, kwa kuwa, ndiyo unaomwezesha mtu kupata ushirikiano mzuri kutoka kwa watu wanaomzunguka.

Ushirikiano huo huwarahisishia watu kupata mahitaji yao muhimu ya kila siku na hivyo kuwa na maisha bora. Kwa kuwa ufugaji wa ng'ombe ni miongono mwa shughuli za kiuchumi kwa Wapare, methali hii, inaonesha kuwa, kugombana na watu kunaweza kumfanya mtu akose mambo muhimu maishani. Hali hiyo inafaninishwa na kukosa ng'ombe ambao hutumiwa kulipia mahari kwa wakwe.
Methali za Kipare zinaihadharisha jamii, kutokana na mambo yawezayo kuleta madhara. Mfano;

*Methali; Hata ethikumoghie, athikushighie momo.*

*Tarijama; Hata ambaye hajakuzaa, asikuwachie laana.*

Laana ni kitu kibaya sana. Laana husababisha matatizo makubwa maishani. Maisha ya aliyelaaniwa huwa ya dhiki duniani na akhera. Mpimaji wa adhabu ya laana ni Muumba Mwenyewe. Binadamu, aombe asiombe, akikosewa na kudhulumiwa, Muumba Hasubiri, Hutowa laana papo hapo.

Dhima ya methali hiyo ni kuihadharisha jamii kuwa, laana ya mtu yeyote aliyedhulumiwa haianguki patupu. Mwenye kukosewa, hulipiwa kwa adhabu ya laana hata kama mkosewa, si mzazi, kwa vile, kila mzazi ni sawa na mwingine.

Laana yake humpata mlaaniwa. Hivyo, ni muhimu kwa watu wote, kuepuka kutenda uovu kwa watu wengine wote, ili kuepuka madhara ya laana. Methali zinatia moyo, kwenye utendaji wa shughuli za kila siku, na zinazowaondolea watu hali ya kukata tamaa. Mfano;

*Methali; Na edhie nyuma, eravusha teri.*

*Tarijama; Hata anayekuwa wa mwisho, hutimua vumbi.*

Kwenye maisha, baadhi ya watu hupata mafanikio kwa haraka kuliko wengine. Wale ambao huchelewa kupata mafanikio, wanapaswa kuwa wavumilivu, kwa sababu hatimaye na wao watafanikiwa kwa kiwango chao, ambacho, Mwenyezi Mungu Atawajaalia. Shuleni, darasani, kijana wa mwisho, kwa kila jaribio, kila mtihani, aliishi, alifanikiwa kuwa Meneja, mwenye magari na tajiri na yule aliyekuwa wa kwanza wa kila somo, kila jaribio, kila mtihani, hata akafika kuwa Profesa, bila ya nyumba, gari wala utajiri wa mali na fedha. Huyo Ndiye Muumba. Dhima kuu ya methali hii ni kuwatia watu moyo, wasikate tamaa. Methali hii, husisitiza kuwa, mwanaadamu anapaswa kutarajia mafanikio, hata kama mafanikio hayo yatapatikana kwa kuchelewa.

**Jedwali Na. 4.4: Juhudi Zinazofaa Kuendelezeya Matumizi ya Methali**

| Idadi ya washiiki | Ambao hawakuelezea juhudi zinazofaa kuendelezea matumizi ya methali | % | Ambao wameelezea juhudi zinazofaa kuendelezea matumizi ya methali | % |
|---|---|---|---|---|
| 253 | 32 | 13 | 221 | 87 |

Watafitiwa 221, ambao ni asilimia themanini na saba (87%), wameeleza juhudi zinazofaa kuchukuliwa ili kuendeleza matumizi ya methali. Juhudi zilizoelezwa ni hizi zifuatazo;

Kuziandika methali kwenye vitabu na majarida. Kuzihifadhi methali kwa muda mrefu bila kupotezwa, kusomwa na watu wa marika yote, kutahakikisha kuwa, methali hizo zinahifadhika kwa njia ya kutumika kwenye maandishi, ili kuendeleza elimu ya jadi, na hivyo, kuimarisha maadili mema ya jamii.

Juhudi nyingine, ni kuongeza matumizi ya methali kwenye maisha ya kila siku. Kwa kawaida, shughuli zinazofanywa kwenye jamii zinahusisha mawasiliano ya lugha. Ni vyema sasa methali zikatumika kwa kiwango kikubwa zaidi, ili kuzifanya zifahamike zaidi, ili kujenga mwamko mpya juu ya matumizi ya methali. Jambo hilo linawezakana, kwa kuwa, jamii inazo methali nyingi ambazo zimefuwawishwa na jamii, mfano wa mbegu ghalani. Kwa kuwa methali ni nyenzo ya kutolea maarifa, zikitumiwa kwa kiwango kikubwa zitaendelea kurithishwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine, na kuiwezesha jamii kuishi kwa kuzingatia mila na dasturi zinazokubalika.

Vile vile, kuna umuhimu wa kuwa na walimu maalumu, ambao wana uweledi kwenye fani ya methali. Walimu hao, kwa kutumia taaluma zao, wasaidie kuzifundisha methali, maana zake, na matumizi yake. Kwa kufanya hivyo, jamii itapata mwamko mpya wa matumizi ya methali na hivyo, kuzirejeshea methali hadhi yake ya asili na ya ziada.

**Jedwali Na. 4.5: Umuhimu wa Kuendeleza Methali**

| Idadi ya washiriki | waliosema hakuna umuhimu wa kuziendeleza | % | Waliosema ni muhimu kuziendeleza | % |
|---|---|---|---|---|
| 253 | 0 | 0 | 253 | 100 |

Kutokana na kielezeo cha jedwali namba 05, watafitiwa mia mbili hamsini na watatu (253), ambao ni asilimia mia moja (100%), wamesema, kuna umuhimu wa kuziendeleza methali kwenye jamii. Kukiri kuwa kuna umuhimu wa kuziendeleza methali, ni ushahidi tosha kuwa, methali zina umuhimu mkubwa kwenye jamii.

Methali ni sehemu ya utamaduni wa jamii, na utamaduni huo, ni lazima uimarishwe na kuendelezwa, kwa kuwa, bila kufanya hivyo, utamaduni utapotea. Matokeo ya kupotea kwa utamaduni ni kujiingiza kwenye utumwa wa tamaduni za kigeni, ambazo kwa hakika, haziendani kabisa na mazingira ya jamii za Kipare. Utamaduni wa Kipare ndiyo wetu. Hivyo, ni muhimu jamii nzima ishiriki kuuendeleza ili kujenga heshima na utu wetu. Tamaduni za Kizungu ni za Wazungu huko kwao Ulaya. Utamaduni wa Mpare ni wa Mwafrika, wa kwetu, Upareni, Afrika. Kila jamii na utamaduni wake kulingana na mazingira yake. Kila Fasihi na Kwao (Sengo 2009).

Vile vile, methali, ni nyenzo ya kuelimishia jamii. Maadili mema ya jamii hufundishwa kupitia matumizi ya methali, mfano;

*Methali; Momo wedi utika ng'ombe he mani.*

*Tarijama; Mdomo mzuri, humpeleka ng'ombe malishoni.*

Kwa kawaida, maneno mazuri humsaidia mtu kupata mazuri, humtoa ng'ombe zizini. Kuongea vizuri na watu, hujenga uhusiano mzuri ndani ya jamii, hujenga heshima na uwaminifu. Mtu akiwa na maneno mazuri, huweza kuwashawishi watu wengine,

kwa ulimi wake mtamu, kuyafanikisha na kuyarahisisha maisha yake ya kila siku, ndani ya jamii. Dhima kuu ya methali hiyo, ni kusisitiza umuhimu kwa watu wote kuwa na kauli nzuri. Kauli nzuri huleta mafanikio kwenye jamii. Hivyo, kila mtu anapaswa kuwa na kauli njema anapowasiliana na watu wengine.

**Jedwali Na. 4.6: Dhima za Methali za Kipare katika Kuendeleza Elimu ya Jadi**

| Idadi ya washiriki | Waliotaja methali bila kueleza kazi zake | % | Waliotaja methali na kueleza kazi zake | % |
|---|---|---|---|---|
| 253 | 17 | 07 | 236 | 93 |

Kwa muda mrefu, methali za Kipare zimekuwa na bado zina dhima ya kuendeleza elimu kwenya jamii ya Wapare. Kazi za methali hizo ni pamoja na:

### 4.3.1 Methali za Kuelimisha

Dhima ya kuelimisha ndiyo inayobeba dhima nyingine ndani yake. Wazee wa Kipare wamekuwa wakizitumia methali kwa kutolea mafunzo yahusuyo jamii katika maisha ya kila siku. Hivyo, methali hutumika kutolea elimu ya namna bora ya kuyaendesha maisha kwa kuzingatia mazingira, mila na dasturi za jamii.

#### 4.3.1.1 Methali; Wekienda kuruka kijevu, uaghane na fae.

**Tarijama; Ukitaka kuruka gema, agana na nyonga.**

Maisha ya kila siku yamezungukwa na vikwazo vingi, kuna wakati mtu hulazimika kuruka akutanapo na vikwazo. Urukaji una miiko yake, isipozingatiwa, mrukaji huweza kupata matatizo makubwa. Kwa asili, Wapare wengi wanaishi sehemu za milimani. Sehemu kubwa ya ardhi yao iko kwenye uwanda wa juu, ambao una miteremko mingi. Sehemu za tambarare ni chache.

Katika maisha, mwanadamu anayo mambo mengi ya kufanya, yawezayo kumnufaisha katika maisha yake. Hivyo, mwanadamu anapaswa kufanya uchaguzi sahihi, wa mambo ya kufanya, kulingana na uwezo aliojaaliwa na Muumba wake. Dhima kuu ya methali hiyo ya Kipare, ni kuwataka wanajamii kuyapima mambo, kujua upana, kina na undani wake ili kujiridhisha kabla ya utendaji. Kufanya hivyo, kunaepusha madhara na khasara inayoweza kutokea, kwa kutofuata uwezekano sahihi wenye kufaa kufuatwa kwenye utendaji. Hivyo, ili kupata matokeo chanya, ni muhimu kuyachunguza mambo kabla ya kuyatekeleza, ili kuyatekeleza kwa kutumia mbinu sahihi. Kabla ya kutenda jambo, ni muhimu kufikiri kwa kina, kupanga na kutafiti na baada ya kuridhika kuwa na uwezekano wa kutenda jambo, ndipo hatua za utekelezaji zianze. Methali hiyo ya Kipare, inasadifu methali ya Kiswahili isemayo;

*Ukitaka kuruka, agana na nyonga.*

#### 4.3.1.2 Methali; Wekivona ithagho, nere kidere

*Tarijama; Ukiona jani kavu la mgomba (sago), lilikuwa changa*.

Maisha ya binadamu yanapitia katika vipindi tafauti. Kuna wakati wa matatizo na furaha, wakati wa utoto, ujana na utu uzima. Kila kipindi, kina raha na karaha zake. Wapare wanaitumia methali hii kumtazama mwanadamu katika safari yake ya maisha. Wakati mwingine huitumia methali hii kwa kusema,

*"Kidere uthimtheke ithagho, ambu naye nere kidere"*

Tarijama; **Jani changa (tumba) usimcheke sago, kwani naye alikuwa jani changa (tumba).** Methali hii inashabihiana na ile ya Kiswahili isemayo:

**"***Kilichompata peku, na ungo kitampata"*

Kumcheka na kumdharau mtu ambaye uwezo wake wa hali au mali umepungua, ni upotofu wa maadili. Hali hiyo huweza kumfika yeyote, wakati wowote. Safari ya maisha ni ghaibu ya Mwenyezi Mungu. Hatupaswi kuchekana kwa mambo magumu tunayokutana nayo maishani.

Majani ya mgomba yanatumiwa katika methali hii. Jani la mgomba linaanza kuchomoza likiwa katika hali ya mviringo na laini. Kisha hujitandaza na kuwa kama mwavuli wa aina fulani. Katika hatua hiyo, huweza kutumiwa na watu wakati wa mvua, kwa ajili ya kujikinga na mvua, ili wasinyeshewe. Hatua ya mwisho, hunyauka na kisha hukauka. Wakati huo, thamani ya jani huwa ndogo. Likiwa katika hatua hiyo ya mwisho Wapare huliita **"ithagho"** kwa Kiswahili, **"sago"**. Jani hilo kavu, kwa wajuao, hulichoma magadi ya jadi ya kupikia, hasa mboga ngumu. Jani, katika hatua yake ya kwanza na ya pili, lina matumizi mengi yanayolifanya liwe na thamani kubwa. Hatua hii inamuwakilisha binadamu akiwa katika kipindi cha neema ya afya, ya akili, ya mali na uwezo mwingi wowote unaompa hadhi kubwa katika jamii anamoishi. Akikosa utu katika kipindi hicho, akawa mwenye ufidhuli na kedi, kwa binadamu wenzake, kutokana na neema alizonazo, watu humtoa thamani.

Dhima kuu ya methali hiyo ni kuwahimiza wanajamii kuwa na busara kwa watu wote, wasiwapuuze na wasiwadharau watu wenye uwezo mdogo. Hakuna mwenye uhakika wa uwezo wake. Inawezekana, leo mtu ana uwezo mzuri, lakini kesho akaamka akiwa hana hili ama lile, uwezo wake wote umepotea. Hivyo, ni muhimu, watu wawe wanyenyekevu kwa wengine bila kujali tafauti zao za kimaisha. Kijana mwenye nguvu, hapaswi kumcheka mzee mkongwe kwa uzee wake. Kijana akumbuke kuwa, mzee naye alikuwa kijana, naye kijana atafikia hatua ya uzee pia.

#### 4.3.1.3 Methali; Vuta vwa mwanake, vuatha nginda

**Tarijama; Upinde wa mtoto, hulenga (hufuma) migomba.**

Utoto ni kipindi chenye shughuli nyingi, ikiwamo michezo ya aina nyingi. Ni katika umri huo, udadisi wa mtoto huweza kusaidia kumgundua kipaji chake kwa kuchunguza mambo anayoyapendelea. Watoto, hasa wa vijijini, hujifunza kuwinda kwa kutumia pinde na mishale, wakiigiza wasasi waliowaona wakienda misituni kuwinda wanyama. Kwa kuwa, umri wao ni mdogo, watoto hufukuzana katika makaazi wanamoishi, wakilenga shabaha kwa kutumia pinde na zana nyingine za kitoto, walizozitengeneza wao wenyewe. Mazingira ya Wapare, ambayo yana migomba, ndiyo yaliyowafanya Wapare kuasisi methali hiyo, ambayo inaeleza, upinde wa mtoto unalenga shabaha kwenye migomba. Watoto hulenga migomba, kwa vile migombani ndiko mashambani. Mshale ukikosa mgomba uliyolengwa, utafuma mgomba mwingine, hautatoka, kumuumiza mtu.

Kwa kuwa ni kichekesho kwa mtu mzima, kuonekana akilenga shabaha migombani, methali hii, inatufundisha kuwa, mtu mzima anatarajiwa kufanya mambo yanayoakisi utu uzima wake. Mambo yakiwa kinyume, atawashangaza wengi. Ikiwa watoto wanalenga migombani, ili wasiumizane, iweje kwa watu wazima, washindwe kuepusha shari zinazojitokeza ndani ya jamii? Watu wazima wanapaswa kuangalia usalama, na kuepusha shari kwa upeo wa mbali zaidi ya ule wa watoto. Ni hali ya namna hiyo, ya mtu kushindwa kufanya mambo sahihi, yanayotarajiwa na watu au jamii yake, ikawasukuma Wapare waone, matumizi ya akili katika masuala yasiyokuwa na tija ni hali duni zaidi kuliko mtoto mwenye upinde akawa analenga shabaha, migombani.

#### 4.3.1.4 Methali; Kiogwe wekikiima moto, kinekuima mbushuke

**Tarijama; Kiazi ukikinyima moto, kitakunyima unga (utamu).**

Maandalizi ya vyakula vingi yanategemea moto, kwa kuchemshia, kukaangia, kuchomea na kuokea. Methali inalinganisha hali mbili katika maandalizi ya chakula. Hali ya kwanza, ni moto mdogo katika uokaji wa viazi. Hali ya pili, ni kukosekana kwa utamu kwa kukosekana moto unaotosha. Kupatikana kwa utamu kunategemea jitihada na maandalizi ya chakula kinachotarajiwa kuliwa.

Katika maisha, mafanikio ya jambo lolote hutegemea jitihada. Kukosekana kwa juhudi za kutosha, kunadumaza mafanikio yanayotarajiwa. Methali hii inafanana na methali ya Kiswahili isemayo;

*"Kula uhondo, kwataka matendo,*

*Asiye matendo, hula uvundo"*

Methali hiyo ya Kipare isemayo, **"Kiogwe wekikiima moto, kinekuima mbushuke"**, inaelimisha kuwa, mafanikio ya jambo lolote hutegemea matumizi mazuri ya juhudi na maarifa. Wale ambao wamefanikiwa, walilazimika kuwa makini katika kuchagua, kupanga na kutekeleza. Pia, walilazimika kufuata sharia, kanuni na taratibu zinazoongoza walichoamua. Kila kitu, kimejengeka kwa kufuata kanuni fulani, zikitimia, kitakuwa kizuri na zisipotimia, hakiwi kizuri. Sharia ni msumeno, inamlazimisha mtu aitekeleze, hata kama haipendi, vinginevyo, mambo hayawezi kuwa.

#### 4.3.1.5 Methali; Kurongora kwa fua, ethiko kumanya vingi

**Tarijama; Kutangulia kwa pua, siyo kufahamu mambo mengi.**

Pua ina kazi ya kunusa harufu. Katika methali hii, pua inatarajiwa iyatambue mambo haraka na kutuma taarifa kwenye ubongo ili hatua stahiki zichukuliwe kukabiliana na tukio. Katika jamii, watu wengi, huamini kuwa, wale waliotangulia kwa maana ya umri, au uongozi, basi wanafahamu mengi. Mafunzo yanayopatikana kwenye methali hiyo ni kuwa, ingawa viongozi hufahamu mambo mengi, kutangulia kwao, si kibali cha kujua mambo yote. Kiongozi si Mtawala, Kiongozi huongoza kwa kuongozwa. Mtawala hufuata kanuni kibubusa. Anaweza kumwuliza baba aliyemzaa, jina na umri wake.

Hakuna mwanadamu anayefahamu mambo yote, hata kama ana umri mkubwa, au hata kama ni kiongozi mkubwa. Ufahamu wa mambo ni mwendelezo endelevu ambao ukomo wake, kwa hapa duniani, ni pale maisha ya mwanadamu yanapofikia ukomo. Mwenyezi Mungu, Muumbaji wa vitu vyote, Ndiye Mwenye sifa ya kujua vitu vyote, Mjuzi wa ya siri na ya dhahiri.

#### 4.3.1.6 Methali; Wekikunda ikoko, ukunde na iova (iua) lakwe

**Tarijama; Ukipenda boga, upende na uwa lake**.

Upendo katika maisha, ni jambo muhimu kwa kila mtu. Upendo humpa mtu faraja awapo na jambo zito linalomtatiza. Matatizo yanatuhimiza kuwa na ndugu, rafiki au mwenza katika kipindi kigumu. Methali hii inasadifu methali ya Kiswahili isemayo "**Ukipenda boga, lipende na uwa lake**" na ile isemayo, "**Ukimpenda jongoo, ipende na miguu yake**"

Uhusiano unaoelezwa katika methali hiyo, juu ya maisha, unahusisha boga, ambalo Wapare wanaliita "**ikoko**" na uwa lake, linaloitwa **iova**. Kuwapo kwa boga ni kuwapo kwa uwa. Hakuna uhalali wa kimoja kukipiga vita kingine kwa kuwa kila

kimoja kinahusika katika kuwapo kwa kingine. Boga hutoa kokwa zinazoendeleza kizazi chake. Makuzi ya mbegu za boga hupitia katika hatua ya uwa. Bila ya kualika uwa, boga haliwezi kumea.

Methali hiyo, ni kielezeo cha upendo wa kweli katika jamii, kwa kuwa, kila mtu, kwa chochote anachokifanya, kiwe kizuri au kibaya, kina athari chanya au hasi kwake na kwa wengine. Ikiangaliwa katika uga wa mapenzi na ndoa, imethibitika kuwa, anayependwa ana mtandao wa watu wengine wanaomhusu, ingawa si katika hilo linalompendezesha. Kumpenda yeye, hakumnyang’anyi haki ya kuwapenda watu wa familia yake. Unachompendea yeye ni sehemu ndogo tu ya duara la upendo. Methali inahimiza kumpenda mtu, wazazi au watoto wake ambao wana aina nyingine za upendo kwake, tafauti na upendo uliyopo baina ya wapendanao.

Wanandoa wote ni wajane watarajiwa, kwa kuwa, mmoja wao, hutarajiwa kutangulia kuiaga dunia. Ikiwa ndoa ilibahatika kupata matunda (watoto), mume au mke atakayeanzisha uhusiano na mjane, atawajibika kwa watoto pia, kwa sababu mshirika wake ana mapenzi ya dhati kwa watoto wake, haki ambayo haiwezi kuondolewa na upendo mpya kwake. Hali iko hivyo hivyo kwa watoto.

Haki ya kumpenda mzazi wao, hainyang’anyiki. Hali hiyo, ndiyo iliyowasukuma Wapare waibue methali hiyo inayowataka wanaopenda, wasibinafsishe aina zote za upendo. Anayefanya hivyo, hufundishwa kuwa, mtu akipeda jambo, apende na mambo mengine yanayolizunguka jambo hilo, vinginevyo, atalikosa jambo hilo. Mpenda kunguni, kapenda na harufu yake.

#### 4.3.1.7 Methali; Wekitegha ifolong'o, vitha ludhighi

**Tarijama; Ukimtega nyani, ficha kamba.**

Kutajwa kwa nyani katika methali hiyo, ni kulinda heshima ya binadamu, kulingana na jambo linalolengwa kuwasilishwa. Nyani ni mnyama anayeishi kwa kutegemea matunda ya porini. Vile vile, anakula mazao yanayostawishwa na wanadamu. Kwa kuwa nyani ni miongoni mwa viumbe ambao hawana urazini, hajui umuhimu wa kuandaa mahitaji atakayoyatumia wakati ujao. Akila sasa na akashiba, hafikirii ya kesho. Wapare hulazimika kulinda mazao yao yasiharibiwe na manyani.

Methali hii, **"Ukimtega nyani, ficha kamba",** imewatumia manyani kuwasema wanadamu wenye tabia kama ya wanyama hao. Katika jamii, kuna matukio mengi yanayozuia kusema ukweli wote unaohusu mambo ya watu. Kuficha kamba ni tafsida inayotumiwa kwa maana ya kuwa mambo ya siri hayafichuliwi hadharani. Ukifanya hivyo, unawapa faida watu wenye nia mbaya, kama alivyo nyani kwa mazao ya binadamu. Ni methali inayotoa hadhari katika kuhifadhi mambo, vitu na hali dhidi ya maadui.

Methali hiyo, inatumika kwenye masuala nyeti na ya siri. Si maarifa yote huwekwa hadharani. Kila mwenye chake, hulazimika kukilinda kwa ustadi mkubwa, ili kisiingie kwenye mikono isiyohusika na kuwanufaisha watu ambao si walengwa. Ulinzi wa aina yoyote una lengo la kuhakikisha kuwa, mhalifu hapati mwanya wa kufanya uharibifu ambao utarudisha nyuma jitihada za mwenye mali, nchi, maarifa, au ujuzi mwingine wowote. Methali inaiona jamii kuwa, inayo hazina ya maarifa muhimu yanayotumika kwa jamii nzima, kinyume cha upotoshaji uliofanywa na

wageni kwa lengo la kuidhoofisha jamii isijiamini ili iwe tegemezi huku ikifanywa nyani, aliyefichiwa Kamba ili asijitambue.

#### 4.4.1.8 Methali; Wekuvithie, kave mghongo uhonze

**Tarijama; Umejificha, kumbe mgongo uko nnje.**

Siyo siri zote, ni siri. Wapare wanaeleza ukweli wa methali ambayo inakejeli watu wafanyao mambo yanayokiuka misingi ya utu, wakiamini kuwa, hawajulikani. Ni methali inayomcheka mtu anayeamini kuwa, mahali alipo amejificha, lakini, hana khabari kuwa sehemu ya mwili wake inaonekana. Methali hiyo inafanana sana na methali ya Kiswahili isemayo,

*"Hakuna siri, ya watu wawili"*

Siri ikihusisha watu zaidi ya mmoja, mtu huyo wa pili hakosi kuwa na mwingine anayemwamini. Imani yake itamsukuma aseme alichosimuliwa au alichokiona na khatimaye, siri, huwa si siri tena. Kama ilivyo kwa fedha zikiwa mfukoni, zitamshawishi anayezimiliki, kuzitafutia matumizi. Kutambua chanzo cha madhara kwa waathirika, ndiko kulikowafanya Wapare waibue methali inayomkejeli mtu aliyejificha huku mgonngo wake unaonekana.

#### 4.3.1.9 Methali; Heliwa, hehirwa

**Tarijama; panapoliwa, hufanywa kazi.**

Maisha mazuri ya wanadamu, hutegemea kuwapo kwa mahitaji yao muhimu, chakula kikiwa ni moja ya mahitaji hayo. Ili mwanadamu aishi, ni lazima apate lishe (chakula). Ukosefu wa chakula, huweza kumfanya binadamu aupoteze uhai wake. Methali hiyo, inahusisha mambo mawili; kuwapo kwa chakula na kufanya kazi.

Hakuna uwezekano wa kukipata chakula kimiujiza tu, lazima wakulima wafanye kazi ngumu ya kukilima mashambani, kukiotesha, kukipalilia, kukivuna na kisha, chakula hicho kuandaliwa na wapishi ili chakula hicho, kiwe tayari kwa kuliwa.

Dhima kuu ya methali hiyo, ni kuwaelimisha wanajamii kuwa, ni lazima kuwajibika kwa kutumia juhudi, maarifa na vipaji. Kuwajibika huko ndiko kutakakowasaidia kupata mahitaji yao muhimu, na kuyaendesha maisha yao, katika hali bora zaidi. Jamii isiyowajibika, haiwezi kukidhi mahitaji yake.

#### 4.3.1.10 Methali; Kiavia cha nkondo, ni kukia

**Tarijama; Maarifa vitani, ni kupona/kushinda.**

Vita ni mapigano baina ya mtu na mtu, makundi ya watu au mataifa. Kwenye uwanja wa vita, kuna kupiga na kupigwa, kujeruhi au kujeruhiwa, kuua au kuuawa. Kwenye vita, kila kundi hupambana na kufa au kupona. Methali hiyo, imetumia vita kuzungumzia matatizo yaliyomo ndani ya jamii. Matatizo ambayo, kila mtu anapaswa kutumia juhudi na maarifa ili kukabiliana nayo. Kwa mfano, kila mtu mwenye akili timamu, huhitaji kujiinua kiuchumi ili kuyaimarisha maisha yake. Kila mtu hana budi kuwajibika kwenye maeneo anayoyamudu, kulinngana na vipaji alivyoruzukiwa na Muumba wake.

Vipaji hivyo, ndivyo vitakavyomwezesha mtu kushinda vita (kuyakabili matatizo), hivyo, kuishi, maisha bora zaidi. Kutokana na kuwapo kwa watu wenye vipaji tafauti vitumikavyo katika kuyaendesha maisha, ndipo Wapare wakaibua methali hii isemayo, “**kiavia cha nkondo, ni kukia**” Tarijama; **“Maarifa vitani, ni kupona/kushinda”,** methali ambayo, huwahimiza watu, kutumia vipaji walivyonavyo, kwa njia za halali, ili kuyakabili matatizo yanayowazunguka.

**4.3.1.11 Methali; Weehia, ethiho wekuia**

**Tarijama; Ukuliapo, sipo uzeekeapo**.

Kwa kawaida, mtu hupitia hatua nyingi za makuzi. Methali hii inaelimisha kuwa, mtu ana ruhusa ya kuzunguka duniani, akijitafutia maisha yake na ya familia yake. Mtu hafungwi kwa kuishi sehemu aliyozawa, hadi kuzeeka.

Kwa sasa, dunia imefungua milango, kila mtu yuko huru, kwenda kokote, kutafuta maisha kwa kadiri awezavyo. Wapare, kama walivyo watu wa jamii nyingine, wamesambaa nchini na nnje ya nchi. Kusambaa kwa Wapare, katika ngazi ya kitaifa na kimataifa, ni kielezea cha uhalisia wa utendakazi wa methali hii ya Kipare.

**4.3.1.12 Methli; Igogo la choo, lethithikia mbungo**

**Tarijama; Gogo la choo, halisikii harufu.**

Jengo la choo ni la huduma muhimu, katika sehemu yoyote ya makaazi ya watu. Katika ujenzi wa vyoo, Wapare huchimba shimo, hupanga magogo na kisha hutandika fito na hatimaye hukandika udongo wa tabaka nene kama sakafu ya choo hicho. Hadi sasa, Wapare wengi, wanaendelea kutumia utaratibu huo wa ujenzi wa vyoo. Methali hiyo, yenye utashihisi, inayapa magogo uwezo wa kutonusa harufu ya uchafu, uliyomo ndani ya shimo. Endapo yangekuwa na uwezo wa kunusa harufu mbaya itokanayo na uchafu huo, yangeamua kuondoka, kuacha kazi ya kukifunika choo.

Wapare huitumia methali hiyo, kuelimisha jamii kuhusu mambo yanayoiharibu jamii. Uharibifu wa mazingira unaofanywa na watu, umeharibu mfumo wa maumbile ya kujiendesha kiasili. Matokeo ya uharibifu huo ni kubadilika kwa tabia ya nchi, joto

limeongezeka, mvua hazitabiriki na majanga mengine kama vile kuharibiwa kwa hali nzuri ya hewa na kukauka kwa baadhi ya vyanzo vya maji. Jamii haina budi kuzinduka, kuchukuwa hadhari katika kukabiliana na mambo ya hatari yanayoiandama jamii.

Licha ya kuwapo kwa vitendo vinavyotishia mustakabali wa jamii, kwa maajabu makubwa, wanajamii wana macho lakini hawaoni, wana masikio lakini hawasikii, wana akili lakini nazo hazitumiki kwa ukamilifu wake. Matokeo ya kupumbazwa huko, kunafananishwa na gogo la choo ambalo, linakaa sehemu yenye harufu mbaya sana, lakini halihisi chochote kuhusu harufu hiyo itokayo shimoni. Kwa hali hiyo linaendelea kudumu katika mazingira ya harufu mbaya hadi litakapoteketea.

#### 4.3.1.13 Methali; Mwana wa nyoka, ni nyoka

**Tarijama; Mtoto wa nyoka ni nyoka.**

Mafunzo makubwa yanayopatikana kwenye methali hiyo ni kuwa, ni jambo la kawaida, kumwona mtoto akiwa na tabia au mwenendo unaoakisi hali za wazazi wake. Wapare huitumia methali hiyo kuelezea kiwango cha mtu au mtoto kurandana na wazazi, kwa sababu za kiurithi wa chembechembe hai zilizomo mwilini. Ikiwa anayefananishwa na huyo mtoto, hakuwa na mapokezi mema, kwa jamii, mtoto mwenye kurithi tabia na mwenendo mbaya, atasababisha jamii iitumie methali hiyo kuikejeli familia hiyo kuwa, hakuna anayeshangazwa na hali hiyo, kwani mtoto wa nyoka ni nyoka

Methali hiyo ya Kipare inafanana na ya Kiswahili isemayo:

*“Maji hufuata mkondo”*.

Methali hiyo, kimaudhui, maji, kufuata mkondo ni sawa na mtoto kufuata mwenendo wa wazazi wake. Jambo hilo ndilo lililowafanya Wapare watunge methali ya “**Mtoto wa nyoka, ni nyoka**”, methali ambayo, ni bia na ile ya Waswahili, **Mwana wa nyoka, ni nyoka**

Haya ndiyo mambo ambayo, (Sengo, 2009, 2016), katika juhudi zake, za kuitakia mema nchi yake, methali nyingi mfano wa hiyo, zikikusanywa na kufanyiwa tarijama, kutoka kwenye makabila, itapatikana Fasihi ya Tanzania kwa Kiswahili, itakayowaonesha kuwa, wanajamii wote ni wamoja, kwa kuwa, methali zina mamoja, yanayofanana na kulingana.

#### 4.3.1.14 Methali; Varethaka vethakaa, nyika irabaki vulavula.

**Tarijama; Wasasi huchakaa, mbuga hubaki vile vile.**

Nyika ni pori linaloota nyasi nyingi, miti michache, mingi ni midogo midogo. Kwa Wapare, neno nyika lina maana, pia, ya sehemu ya mbali na nyumbani. Wote wanaokwenda kutafuta maisha nnje ya mahali walikozaliwa, husemwa wako nyikani. Maana nyingine ya nyika ni mbuga au msitu uliyoko mbali na makaazi ya Wapare. Maana hii ya mwisho ndiyo iliyokusudiwa kwenye methali hiyo. Kwa Kiswahili, NYIKA ni pori, masafa marefu ya pori, ndipo tukawa na nchi kubwa ya Tanga, Tanga + Nyika = Tanganyika (Sengo, 2016).

Kwa kawaida, wawindaji, hupata mahitaji yao katika misitu. Ardhi inayostawi msitu unaovutia makaazi ya wanyama wanaowindwa, inabakia kama ilivyo. Vizazi na vizazi hufanya shughuli zao katika ardhi au misitu hiyo, lakini ardhi au misitu huendelea kubaki kwa ajili ya vizazi vingine. Mwanadamu anapaswa kuwa na

hadhari, kwa kuepuka kufanya mambo ambayo hatimaye humletea madhara yeye mwenyewe, si kwa kudhani anafanya kwa kumkomoa huyu ama kumdhalilisha yule, ikiwa anayoyafanya si ya sawa, mtenda wa hayo hudhalilika yeye mwenyewe. Mtu akifanya mambo yasiyo tija, hujiumiza mwenyewe. Waswahili husema

*"Mwenda mbizi nchi kavu, huupujua usowe"*

Methali hiyo, ina matumizi mapana yanayojumuisha shughuli nyingine nyingi. Wakulima huitumia ardhi hiyo hiyo, ambayo ilikuwapo miaka mingi iliyopita. Vizazi vingi vimepita na kupata mahitaji yao. Muda wa uhai wao ulipomalizika, vizazi hivyo vilitoweka, na kuiacha ardhi hiyo ikiendelea kutoa huduma kwa waliopo sasa.

Matumizi mabaya ya ardhi yana madhara kwa wanaoitumia. Hivyo, methali hii, inawakejeli wale wanaoitumia ardhi vibaya, kuwa, ni wao watakaoyakosa matunda bora kwa kutoilea ardhi vizuri. Kwa hali hiyo, Wapare huitumia methali hii kujielimisha kuwa, ni upuuzi, kutumia kitu vibaya ili hali kitu hicho kina faida kwao. Chenye manufaa, ni vizuri kukitunza, kwa faida ya kizazi cha sasa na kijacho.

### 4.3.2 Methali Zinazohimiza Uwajibikaji

Uwajibikaji ni dhima nyingine ya methali, inayowasisitiza watu kufanya kazi kwa juhudi na maarifa yao yote ili kupata maendeleo. Mtu anapowajibika, huepuka uvivu ambao ni sumu ya maendeleo;

#### 4.3.2.1 Methali; Eomba mbogha, ena yakwe yeghaghie

**Tarijama; Aombaye mboga, ana yake iliyochacha**.

Siku hazilingani. Maisha ya familia nyingi zisizo na uwezo wa kujikimu, kuomba hiki na kile ni jambo la kawaida. Methali hii inamlinganisha mtu anayekwenda

kuomba mboga kwa jirani, na yule mwenye ya kwake, ambayo imechacha. Hata kama analazimika kwenda kuomba, basi anapaswa kuwa na mipango iliyo kamili ya kuweza kumsaidia, kukabiliana na shida yake ikiwa maombi hayo, kwa jirani yake, yatagonga mwamba. Methali hiyo, inasadifu zile za Kiswahili zisemazo:

*"Ukibebwa, ujikaze"*

*"Ukishikwa, shikamana"*

Nchi zinazoendelea, zisitegemee kuomba kwa ajili ya maendeleo ya watu wake. Nguvukazi na rasilimali zilizopo zitumike, kikamilifu, kwa kuwahamasisha watu wao, kuwajibika ipasavyo. Badala ya bajeti ya nchi kuwategemeza wahisani kwa kila kitu, mboga zilizochacha, zitumike kikamilifu, katika sekta zitakazosisimua uchumi wa nchi. Wataalamu na wanaharakati wanaoitakia nchi mema, wasikilizwe badala ya kuwaacha mafisidi kuendelea kuzihujumu nchi zao.

Methali hiyo, inaona ubaya wa kuombaomba, ambako kunahatarisha uhuru, utu na heshima ya taifa. Mambo ya msingi katika uendeshaji wa jambo lolote la ndani ya jamii zetu, hayahitaji maarifa kutoka nchi za nnje. Maarifa yote yenye umuhimu mkubwa, yamejaa katika amali za fasihi zetu za asili. Nchi ni nchi, zisiitwe za Ulimwengu wa tatu. Tuwache kuwa manyani wasioona mamando yao. Wakitazama nyuma kwa wenzao, watayaona na ya kwao. Nchi ijifanyie mambo yake yote, yenyewe. Kama ipo iliyojifanyia ikawa NCHI HISANI, kwa nini na nchi nyingine zisijifanyie zikajitegemea badala ya kuwa tegemezi? Methali hiyo, inapiga mbiu ya kutuamsha, tujitambue kuwa, sisi ni matajiri, tusiojijua. Tuzindukane na usingizi wa pono. Tujifanyie yetu, tujikomboe kiuchumi.

#### 4.3.2.2 Methali; Mwana wa mkiva, ethibanda (ething'enda)

**Tarijama; mtoto wa mkiwa, hanenepi.**

Methali hii, inaeleza hali duni ya maisha, katika familia. Mataifa yaliyoendelea yamekuwa na ukiritimba wa kuyafanya mataifa yanayoendelea yaamini kuwa, kuendelea ni kufanana na wao. Dhanna hii ni dhaifu sana. Huwafanya wananchi wasiwe na mawazo huru yanayozingatia uwezo, hali na mazingira yao. Mfano mzuri wa tajriba ya maisha ya wanyonge wa Kisudani, Khartoum, mikate mizuri iliaminika kuwa ni ya Wazungu (Sengo 1978 – 1985). Ili kuiepuka hali ya tafauti kiuwezo wa kiuchumi, ni lazima mamlaka zinazoongoza na kusimamia mifumo ya rasilimali katika ngazi za taifa, ziwajibike kwa kupiga vita, hali hiyo ya uonevu ili kuleta uwiano unaolingana katika nyanja zote za maisha.

Methali hii, **"Mtoto wa mkiwa, hanenepi"** inathibitisha ukweli kuwa, wanyonge hawana chao kwenye jamii nyingi za kifisidi. Hawawezi kupata mahitaji yao ya msingi kama ilivyo kwa matajiri. Hali hii ndiyo inayofananishwa na wazazi, kushindwa kuwalisha watoto wao, maishani. Hivyo, ni muhimu kwa jamii, kuangalia namna bora ya kugawana rasilimali zilizopo ili kila mmoja aishi kwa raha kwenye nchi yake.

#### 4.3.2.3 Methali; mrerokia nkemo, ni mrerokia kula

**Tarijama; Anayewahi kazini, ndiye anayewahi kula.**

Kufanya kazi kwa juhudi, maarifa na kwa wakati, ni jambo muhimu sana kwenye maisha ya mwanadamu. Uzembe kwenye kazi ni chanzo kikuu cha kushindwa kupata mafanikio yanayotarajiwa katika maisha. Hata methali ya Kiswahili nayo husema hayo hayo *"Ajizi, nyumba ya njaa"*

Dhima kuu ya methali hii, ni kuhimiza uwajibikaji. Methali inahusisha mambo ya kuwahi kazini na kuwahi kula. Kutokana na mafunzo yanayopatikana, anayefanya kazi kwa juhudi, maarifa na kwa kuzingatia muda, ndiye apataye fursa ya kuufikia ufanisi na kwa haraka zaidi, hivyo, kuweza kujikimu kistahiki, kula vizuri, kuvaa vizuri na kulala pazuri. Mtu akiwa mzembe, asiyeutumia vyema muda wake, juhudi zake, na maarifa yake katika kufanya kazi zake, hawezi kuyafikia mafanikio hayo kwa ufanisi.

### 4.3.3 Methali za Kuwatakia Watu Kheri na Baraka

Mtafiti amekusanya methali za kutakiana kheri na baraka ndani ya jamii. Baadhi ya methali hizo ni:

**I. Baraka kwa wanandoa na familia**

**4.5.3.1 Methali; Wekinkwa iziko, uvoke na wavuta**

**Tarijama; Unapoanza unyumba, mzawa wa kwanza awe wa upinde.**

Methali hii hutumika wakati wa ndoa. Ni methali ya kuwatakia wanandoa baraka ya watoto wa kiume na watoto wa kike. Methali hii, husemwa kwa Bibi harusi, siku anapoagwa nyumbani kwao. Wazazi wachache wenye busara, hupawa fursa ya kutoa maneno ya busara, ya kumtoa Bibi harusi kwa ajili ya kwenda kwa Bwana harusu.

Maneno yanayotumika kwenye methali hii, si ya moja kwa moja, ila ni ya uficho. Badala ya kusema mtoto wa kiume, husemwa "**uvoke na wavuta**". Wote walioketi katika kikao hicho wataelewa, "mtoto wa kiume", kwa vile katika mila na dasturi za wahenga, upinde ni silaha inayoshikwa na kina baba. Wakati mwingine Wapare husema: *"…, uvoke na enekujia kampombe"*

Waliposema, “**uvoke na enekujia kampombe**”, kwa maana ya mtoto wa kike, ambaye kwa mgawanyo wa kazi kwenye jamii ya Wapare, mtoto wa kike humsaidia mama, kazi za nyumbani. Kwa sehemu kubwa, Wahenga wa jamii ya Wapare, walipendelea kifungua mimba awe wa kiume na wa kike afuate. Wahenga walipenda watoto wa jinsia zote kutokana na umuhimu na nafasi zao katika familia au jamii kwa jumla. Mtoto wa kiume alitajwa mwanzo, kwa vile ndiye mrithi, walii na mlezi wa familia, ikitokea, baba katangulia Kuzimu.

#### 4.3.3.2 Methali; Udhime iyo kaa wetonga, na kitangu na ighembe

**Tarijama; Uisimamie hiyo familia unakoolewa, kwa sahani na jembe.**

“**Kitangu**” ni chombo asilia, kama sahani za siku hizi, iliyotengenezwa kwa ufundi stadi wa asilia, kwa kutumia majani (nyasi) na kamba za katani. Chombo hicho kilikuwa cha kulia chakula. Siku hizi chombo hicho, hakitumiki tena kwa kulia chakula. Siku hizi, hutumika zaidi, kuhifadhia matunda, na wengine hukitumia chombo hicho, kama pambo.

Methali hiyo, iliposemwa kwa binti aliyeolewa, ilimtakia kheri na baraka. Kwa mila na dasturi za Wapare, msichana alipoolewa alipawa jembe, panga, na shoka, ili atambue kuwa, baraka ya nyumba itakuja, si kwa uzazi wa watoto tu, bali kwa kufanya kazi, kwa bidii, ili nyumba iwe na baraka ya mali na chakula. Uvivu ni sumu ya maisha. Maisha ya ndoa ndiyo maisha halisi ya kupokezana vijiti vya vizazi.

Hivyo, kazi ni lazima zifanyike kwa juhudi na kwa maarifa makubwa. Kutokana na mabadiliko kwenye jamii, siku hizi wakati wa kuagwa, msichana husemewa,

"Nakuinga kalamu, itumie nenzo"

Tarijama; Nimekupa kalamu, uitumie vizuri.

Elimu ndilo **jembe** la msichana huyo,

"**Udhime iyo kaa na ighembe**"

**Tarijama; Uisimamie hiyo familia kwa jembe.**

Kwenye hiyo nyumba, kusiwe na ukosefu wa chakula. Neno NJAA lisipawe nafasi. Njaa, ndani ya familia ni aibu.

**4.3.3.3 Methali; Nyumba ifuke mushi, ikete ng'ombe na vantu**

**Tarijama; Nyumba ifuke moshi, iwe na ng'ombe na watu**.

Kiasili, Mpare, anapomaliza ujenzi wa nyumba, hufanya sherehe ya kuhamia. Chakula maalumu hupikwa, hasa viazi vikuu, pamoja na pombe ya miwa. Mzee wa mji, kiongozi wa boma, hufanya tambiko na kufungua nyumba ili iwe tayari kuishi watu.

Siku hiyo ya kuhamia, ng'ombe huingizwa ndani, na moto huwashwa kwa mara ya kwanza kwenye mafiga, katika nyumba na mkuu wa mji, husema maneno yafuatayo,

"**Yoo nifuta moto he ii nyumba, nyumba ifuke mushi, ikete ng'ombe na vantu, na moto usifwe he ii kaa, hasisoveke kijo, nzota iikae hae na ii kaa**.

**Tarijama; "Nawasha moto kwenye hii nyumba, ifuke moshi, isikose chakula, iwe na ng'ombe na watu, na iwe na neema za kila namna"**

Kwa maneno hayo, nyumba hufunguliwa rasmi. Hiyo ni ibada fupi, tambiko, katika jumla ya itikadi za kisanaajadiiya. Muumba Hupokea duwa hizo na Hutoa baraka

katika nyumba mpya.Wahenga wa Kipare hutegemea vitu vitatu muhimu kwenye nyumba, watu, mifugo, na chakula chao. Nyumba ikikosa mambo hayo, ilionekana sawa na kihame.

**II. Baraka kwa wasafiri**

Ni jambo la kawaida kwenye jamii, watu kusafiri, kwa ajili ya kukidhi mahitaji yao. Wapare hutumia methali, ambazo, ni kama dua za kuwatakia baraka wasafiri.

#### 4.3.3.4 Methali: Uthekiwe, uko hantu wetonga

**Tarijama; Upokelewe kwa kicheko, huko uendako.**

Methali hii, hutumika kumtakia baraka anayesafiri kwenda mahali. Kwa mfano, kuwasalimia rafiki, au kwenda sokoni. Methali hii, ni ya kumwombea msafiri akutane na watu wazuri, huko aendako. Watu ambao, watampokea na kukaa naye vizuri, hadi muda wa kuachana nao ukifika. Kama mtu anakwenda kufanya biashara, methali hii hutumika kumuombea, apate wanunuzi wa bidhaa zake, tena wanunuzi watakaozinunua bidhaa hizo bila manung'uniko.

#### 4.3.3.5 Methali; Tonga, uvate nguru mutwi

**Tarijama; nenda ubahatike kumkanyaga kobe kichwani**.

Kwa kawaida, kobe ni mnyama mpole. Anaweza kukamatwa na kuwekwa begani au kichwani. Kobe aonapo adui, hukificha kichwa chake ndani ya gamba lake. Si rahisi, mtu kukikanyaga kichwa cha kobe. Mtu kukikanyaga kichwa cha kobe, huchukuliwa kuwa ni jambo kubwa na lisilo la kawaida. Methali hii, hutumika kumtakia mtu baraka ambayo ni nadra sana kupatikana.

### 4.3.4 Methali za Kuwatakia Laana Watendao Maovu

Tangu zamani, Wapare wamekuwa wakitumia methali zenye maneno mazito. Baadhi ya methali zina maneno mazito, na methali humfanya mwenye kutamkiwa, kubadili mwenendo wake mbaya, na kufuata maadili mema. Methali hizo zilitumika na bado zinatumika kama fimbo au silaha, ya kujihami dhidi ya uonevu, dhuluma na unyanyasaji kwa wanyonge. Kiasili, Wapare huogopa sana laana kwenye maisha yao. Hujihadhari sana wasipate laana, hata ya kuombewa na wapita njia. Hii ni kwa sababu, Wapare huamini, hata laana ya mpita njia, huweza kumpa mtu mateso. Wapare husema;

**“Hata ethikumoghie athikushighie momo”.**

**Tarijama; Hata asiyekuzaa, asikutakie laana.**

Laana mbaya si ile ya mzazi tu, hata ya mtu mwingine yaweza kuleta madhara. Kwa kiasi kikubwa, uwaminifu umejengwa katika misingi ya khofu, ili mtu asimdhulumu mwingine, akiamini kuwa, anaweza kulaanika, afe au kupata tabu na mateso yeye na familia yake au ukoo wake. Mafunzo hayo yamewafanya Wapare wengi kuwa watu wapenda amani na usuhuba mwema na wengine.

#### 4.3.4.1 Methali: Thomwa ni kibathi cha Mghara

**Tarijama; Chomwa kwa kijiti cha Mghara.**

Mghara ni aina ya mti mgumu uotao nyikani, Upareni. Kijiti cha Mghara, kikiingia mwilini, kinatoboa kama kisu, na kidonda chake huchelewa sana kupona. Lugha inayotumika kwenye methali hiyo, si ya moja kwa moja, bali ni lugha yenye uficho. Methali hiyo hutumiwa na watu waliotendewa ubaya na wakawa hawana njia

nyingine ya kujitetea. Hivyo, watu waliotendewa ubaya, na hawana njia nyingine, huitumia methali hiyo kama fimbo dhidi ya wabaya wao. Wabaya hukabidhiwa kwa Mungu, kwani hiyo ndiyo fimbo ya uhakika ya mnyonge.

Kwa jumla, methali hiyo, hutamkiwa mtu, kwa lengo la kumtakia mtu huyo, apatwe na mambo mabaya yatakayomtesa kwa muda mrefu. Mabaya hayo huwa ndiyo malipo ya ubaya wake. Mara nyingi, baada ya kutamkiwa maneno hayo, wazee wenye busara humkalisha chini aliyefanya kosa na kumshauri aende kumwangukia mgomvi wake kwa kumwomba msamaha aliyekosewa. Lengo likiwa, ni kuiondoa khatari inayoweza kujitokeza kutokana na laana hiyo. Asipoomba radhi, humkuta, lake na nduguze. *"Mchuma janga, hula na wakwao"*

#### 4.3.4.2 Methali; Uome tha lugwi

**Tarijama; Ukonde, kama kinyonga.**

Kinyonga ni kiumbe mwenye sifa ya kipekee. Kinyonga huweza kujibadili rangi kulingana na mazingira yanayomzunguka. Pamoja na sifa hiyo ya kujibadilisha rangi, kinyonga ana umbo dogo. Umbo ambalo, hakuna wakati ambapo linaweza likapawa sifa ya unene. Dhima kuu ya methali hii, ni kuwatakia laana watu waovu, wapate ukata mkubwa na pia afya mbaya, kutokana na udhalimu walioutenda. Mara nyingi, methali hiyo, hutumiwa na watu walioibiwa fedha au mali. Mtu, huweza kuitumia methali hiyo, pindi aonapo dalili ya kudhulumiwa mali zake. Mtu aliyedhulumiwa, huweza kutoa onyo kwa kusema:

"**Mwekighuha mari jangu, muome tha lugwi"**

**Tarijama; "Mkichukua mali zangu, mkonde kama kinyonga"**

Maana yake ni kuwa, kama mtachukua mali zangu , basi dhiki kubwa ikukabilini, msipate faraja yoyote kwa ubaya mliyoutenda.

Methali hiyo itumikapo, mara nyingi, husaidia kuwaogopesha watu wenye nia ya kuwadhulumu wengine, na wale ambao wameshadhulumu, huweza kuomba msamaha na kuzirejesha mali walizozidhulumu. Kwa njia hiyo, elimu ya jadi kuhusu madhara ya laana, huendelea kurithishwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine na hivyo, kuendelea kulinda na kuyaendeleza maadili mema ya jamii.

**4.3.4.3 Methali; Nanga ubuka, tha Kiramba**

**Tarijama; Upasuke, kama tunda la Mkweme.**

Mkweme ni aina ya mmea. Mmea huo huzaa matunda, ambayo, yanapokomaa, hupasuka na kutoa kokwa. Kokwa hizo hutumiwa kama kiungo cha chakula. Maneno ya methali hiyo ni maombi ya laana ya kumtakia mtu mabaya. Yaani tumbo lake livimbe na kuwa kubwa, kisha, lipasuke kama tunda la Mkweme.

